AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

BARAZA LA UTENDAJI
Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na nne
15 Januari - 15 Februari 2024
Addis Ababa, ETHIOPIA

EX.CL/1464(XLIV)
Asili: Kiingereza

RIPOTI YA KAMATI NDOGO KUHUSU NEPAD

RIPOTI YA MWAKA YA KAMATI NDOGO YA WAWAKILISHI WA KUDUMU (PRC) KUHUSU NEPAD KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI DESEMBA 2023

UTANGULIZI

1. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD, (hapa inajulikana pia kama Kamati Ndogo), ilionyesha dhamira thabiti katika kutekeleza shughuli zake kwa mwaka mzima wa 2023. Katika kipindi kinachoangaziwa, Uenyekiti wa Kamati Ndogo ulikabidhiwa kutoka kwa **Mhe. Mohamed Lamine Laabas**, Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, na kwenda kwa **Mhe. Victor Adekunle Adeleke**, Balozi wa Shirikisho la Jamhuri ya Nigeria.

2. Zaidi ya hayo, kufuatia uteuzi wa Mhe. Victor Adekunle Adeleke kama Mkuu wa Itifaki wa Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria mnamo Mei 2023, Uenyekiti wa Kamati Ndogo ulichukuliwa na Mhe. Abdi Mahamoud, Balozi wa Jamhuri ya Djibouti, Makamu wa Kwanza wa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo.

3. Katika kipindi cha mwaka mzima, Kamati Ndogo ilifanya mikutano ya mara kwa mara ambapo ilipokea taarifa kuhusu hali ya utekelezaji wa programu zinazohusiana na AUDA-NEPAD. Taarifa hizo fupi ziliwasilishwa kwa pamoja na AUDA-NEPAD na Maafisa wa Kamisheni pamoja na wadau wengine husika pale ilipohitajika. Zaidi ya hayo, kupitia kwa Mwenyekiti wake, Kamati Ndogo ilishiriki katika shughuli nyingine, ikiwa ni pamoja na vikao vya Kamati Maalumu ya NEPAD.

4. Mwaka 2023, muundo wa Kamati Ndogo ulibaki kama ifuatavyo:
    - **Kamati Tendaji**: Nigeria (Mwenyekiti); Djibouti (Makamu Mwenyekiti wa 1); Kongo (Makamu Mwenyekiti wa Pili); Botswana (Makamu Mwenyekiti wa 3); Algeria (Mwandishi)
    - **Wajumbe**: Burundi; Guinea ya Ikweta; Ghana; Lesotho; Madagaska; Mauritania; Niger (Imesimamishwa); Rwanda; Senegal; Zambia.

5. Ripoti hii inatoa muhtasari wa shughuli zilizofanywa na Kamati Ndogo ya NEPAD katika mwaka mzima wa 2023 na inatoa mapendekezo ya kuongeza msaada kwenye utekelezaji wa programu za AUDA- NEPAD na, kwa kiasi kikubwa, Ajenda 2063.

I. MUHTASARI WA SHUGHULI ZA KAMATI NDOGO YA NEPAD KWA MWAKA 2023.

A. Shughuli za Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya NEPAD kwa niaba ya Kamati Ndogo.

6. Kwa mujibu wa Kanuni ya 3 ya Kanuni za uendeshaji wa Kamati Maalumu ya NEPAD, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo Mhe. Mohamed Lamine Laabas alishiriki katika mkutano wa 67 wa Kamati Maalumu ya AUDA-NEPAD ambao ulifanyika

tarehe 7-8 Februari 2023 katika muundo wa mseto. Mkutano huo uliongozwa na **Mhe. Diyana Gitera**, Mshauri katika Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Rwanda na **Mhe. Gnouka Diouf**, Mshauri wa Mawaziri wa Rais wa Jamhuri ya Senegal na Waziri wa Masuala ya Uchumi.

7. Kamati Maalumu ilichunguza ripoti ya mwaka ya AUDA-NEPAD ya mwaka wa fedha 2023 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa masuala ya kimkakati kama ifuatavyo:
   I. Mkutano wa 2 wa Wakuu wa nchi na serikali kuhusu Ufadhili kwa Maendeleo ya Miundombinu uliofanyika Dakar
   II. Nishati kwa bara la Afrika
   III. Ufadhili wa sekta ya Afya na Hatua endelevu za Kutokomeza UKIMWI na Magonjwa Yanayoambukiza na Yasiyo ya Kuambukiza
   IV. Muongo wa pili wa Ajenda 2063
   V. Masuala Matatu muhimu kuhusu Amani, Usalama na Maendeleo

8. Makamu Mwenyekiti wa Kwanza wa Kamati Ndogo **Mhe. Balozi Abdi Mahamoud** alishiriki katika Mkutano wa 68 wa Kamati Maalumu ya AUDA-NEPAD uliofanyika kuanzia tarehe 31 Oktoba - 1 Novemba 2023 huko Johannesburg, Afrika Kusini.

9. Mkutano huu uliongozwa na **Mhe. Balozi Ashraf Swalam**, Mwakilishi Binafsi wa Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, na **Mhe. Balozi Youssouf Assoumani**, Balozi wa Muungano wa Comoro, Mwenyekiti wa PRC. Kamati Ndogo iliwakilishwa na Kaimu Mwenyekiti wake, **Mhe. Balozi Abdi Mahamoud**, **Mhe. Balozi Daniel Owassa**, Makamu Mwenyekiti wa 2 na Mhe. **Balozi Lamine Laabas**, Mwandishi wa Kamati Ndogo.

10. Katika mkutano huo, Kamati Maalumu ilipokea taarifa kuhusu hali ya utekelezaji wa Programu zifuatazo za AUDA-NEPAD:
    I. Mpango wa Kwanza wa Utekelezaji wa Miaka Kumi
    II. Rasilimali Watu na Maendeleo ya Kitaasisi
    III. Miundombinu
    IV. Sayansi, Teknolojia, na Ubunifu
    V. Kilimo, Usalama wa Chakula na Uendelevu wa Mazingira

B. <u>Mkutano wa pamoja kati ya AUDA-NEPAD na Kamati Ndogo ya AUDA-NEPAD.</u>

11. Kamati Ndogo ilifanya mkutano wake wa kila mwaka na AUDA-NEPAD katika makao makuu yake huko Midrand, Afrika Kusini kuanzia tarehe 13 hadi 14 Machi 2023. Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa kujadili masuala muhimu kuhusiana na maendeleo katika utekelezaji wa majukumu na programu za Taasisi hiyo. Mkutano huo uliongozwa na **Mhe. Balozi Mohamed Lamine Laabas**, Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD.

12. Wakati wa mkutano, Mkurugenzi Mtendaji wa AUDA-NEPAD, **Mhe. Nardos Bekele-Thomas** aliwasilisha muhtasari wa kina wa lengo la mpango mkakati kwa kipindi cha mwaka 2022-2024. Alisisitiza juhudi za ushirikiano kati ya AUDA-NEPAD na Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC) katika kutathmini muongo wa kwanza wa Ajenda 2063 na kuandaa mpango wa pili wa utekelezaji wa Miaka Kumi. Pamoja na hayo, Wakurugenzi wa AUDA-NEPAD waliwasilisha mada kuhusiana na masuala mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

    I. Kilimo, Usalama wa Chakula na Uendelevu wa Mazingira.
    II. Miundombinu, Biashara na Viwanda.
    III. Rasilimali Watu na Maendeleo ya Kitaasisi.
    IV. Mpango Mkakati, Bajeti, na Uendeshaji.

13. Kufuatia mawasilisho yaliyofanywa na Mkurugenzi Mtendaji na Wakurugenzi wa AUDA-NEPAD, wajumbe wa Kamati Ndogo walitoa mapendekezo yafuatayo:

    a. Kamati Ndogo iligusia wasiwasi kuhusu uratibu, ikiitaka AUDA-NEPAD kushughulikia suala la kuongeza juhudi kati ya AUDA-NEPAD na idara/Mashirika mengine ya UA, pamoja na haja ya kuimarisha ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika.
    b. Kuhusu suala la kilimo, msisitizo uliwekwa kwenye jukumu la AUDA-NEPAD katika kutekeleza Mipango ya Kitaifa ya Uwekezaji kwenye Kilimo, na ombi la kupewa taarifa kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Mkataba wa Malabo.
    c. Kuhusu suala la nishati barani Afrika, Kamati Ndogo ilisisitiza haja ya ushiriki wa vijana, umiliki wa Nchi Wanachama, na kupendekeza mkakati wa mawasiliano.
    d. Umuhimu wa uelewa wa kitaifa kuhusu Ajenda 2063 ulitambuliwa, pamoja na ombi la msaada wa AUDA-NEPAD katika kuimarisha mwonekano.
    e. Kuhusu miundombinu, Kamati Ndogo ilitaka ufafanuzi kuhusu utaratibu wa utekelezaji wa azimio la Dakar.
    f. Kuhusu uendeshaji, AUDA-NEPAD ilihimizwa kutafuta msaada kutoka kwa Nchi Wanachama ili kuajiri wataalamu mahususi kutokana na uhaba wa wafanyakazi na fedha.

C. <u>Mikutano ya Kamati Ndogo</u>

14. Mwaka 2023, Kamati Ndogo iliendesha jumla ya mikutano 9, kuanzia mkutano wa 34 hadi wa 42.

15. Mkutano wa 34 ulifanyika kwa njia ya mtandao tarehe 19 Aprili 2023, mkutano huo ulijikita kwenye kupitishwa kwa mpangokazi wa kila mwaka wa Kamati Ndogo wa mwaka 2023, na kukabidhiwa Uenyekiti wa Kamati Ndogo kutoka kwa **Mhe. Mheshimiwa Mohamed Lamine Laabas**, Balozi wa Algeria, na kwenda kwa **Mhe. Victor Adekunle Adeleke**, Balozi wa Nigeria.

16. Mkutano wa 35, ulifanyika tarehe 8 na 10 Mei 2023 katika makao makuu ya AUC, chini ya Uenyekiti wa **Mhe. Balozi Victor Adekunle Adeleke** ili kujadili mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2024 yaliyotolewa na AUDA-NEPAD na Kitengo cha Uratibu cha AUC AUDA-NEPAD.

17. Wasilisho la rasimu ya bajeti ya AUDA-NEPAD 2024 lilifanywa na Mkuu wa Wafanyakazi wa AUDA-NEPAD, **Dkt. Msingathi Sipuka**, na Bw. Mohamed Abdisalam, Mkurugenzi wa Uendeshaji. Wakati wa uwasilishaji, AUDA-NEPAD ilitenga bajeti ya Dola za Marekani milioni 15.1, ambazo zilikusudiwa kupatikana kutoka kwenye michango ya Nchi Wanachama na Dola za Marekani milioni 35 zilipendekezwa kutoka kwa fedha za Wabia wa Maendeleo. Ni muhimu kutambua kwamba kutokana na vikwazo vilivyopo vya ukomo wa bajeti, michango ya Nchi Wanachama wa AUDA-NEPAD ilipunguzwa hadi Dola za Marekani milioni 8.1.

18. Bw. Mohamed Abdisalam alijikita kwenye vipaumbele muhimu vifuatavyo vya bajeti ya AUDA-NEPAD ya 2024 kama ifuatavyo:
    i. Kilimo, Usalama wa Chakula na Lishe na Uendelevu wa Mazingira (CAADP, Chakula Shuleni)
    ii. Rasilimali Watu na Maendeleo ya Kitaasisi (SIFA, Nishati barani Afrika, Ufadhili wa Sekta ya Afya, Elimu ya Sayansi, Teknolojia na Hisabati)
    iii. Miundombinu, Biashara na Viwanda
    iv. Mageuzi ya Kitaasisi na Utawala Bora
    v. Sayansi, Teknolojia na Ubunifu
    vi. Masuala tatu muhimu (Amani, Usalama na Maendeleo)

19. Zaidi ya hayo, **Bw. Mohamed Abdisalam** alijikita kwenye dhamira ya AUDA-NEPAD katika utekelezaji wa programu zake, akionyesha ongezeko kubwa la viwango vya utekelezaji wa bajeti kutoka 95% mwaka 2021 hadi 98% mwaka 2022.

20. Kutokana na mawasilisho ya bajeti ya AUDA-NEPAD, Kamati Ndogo ilitoa mapendekezo yafuatayo:

    a) **Kutumia Mbinu Inayotegemea Matokeo**: Pendekezo ni kuifanya bajeti ya AUDA-NEPAD 2024 iwe na matokeo zaidi, ikionyesha wazi mchango wa ufadhili wa Nchi Wanachama kwenye bajeti na uendeshaji.
    b) **Utafutaji Makini wa Rasilimali**: AUDA-NEPAD inashauriwa kutafuta vyanzo bunifu vya ufadhili, hasa kwa kuzingatia muundo wake wa sasa wa ufadhili ambapo 33% kutoka Nchi Wanachama na 67% kutoka kwa Wabia wa Maendeleo.
    c) **Kuepuka Kurudia rudia**: Mkazo uwekwe katika kuzuia kurudiwa rudiwa kwa juhudi kati ya AUDA-NEPAD na idara/shirika nyingine za UA.
    d) **Mapitio ya Bajeti ya Sayansi na Teknolojia**: Kuna pendekezo la kupitiwa kwa bajeti ili kuoanisha rasilimali na lengo mahususi, ikizingatiwa

kutokuwepo usawa kati ya mgao wa Sayansi na Teknolojia na Miundombinu, Biashara na Viwanda.

e) **Ripoti kuhusu Mkutano wa Dakar kuhusu Ufadhili wa Miundombinu**: AUDA-NEPAD inapaswa kuandaa na kuwasilisha ripoti ya kina kuhusu Mkutano wa Dakar wa 2022 kuhusu ufadhili wa Miundombinu, kushughulikia masuala yaliyobainishwa na Nchi Wanachama.

f) **Uwazi kuhusu Mamlaka na Shughuli**: Mkutano unapendekeza kutolewe ufafanuzi kuhusu mamlaka na shughuli za AUDA-NEPAD, kubainisha tofauti kati ya Idara na Vyombo vingine ya UA.

g) **Mfumo wa Bajeti ya Miaka Tofauti**: AUDA-NEPAD inahimizwa kuweka mfumo wa bajeti wa miaka tofauti, kuweka kigezo kwa Vyombo na idara nyingine za UA ili kufuata.

21. Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uratibu, Bibi Aïssatou Hayatou, aliwasilisha bajeti ya 2024 ya Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD. Katika wasilisho lake alijikita kwenye vipaumbele vifuatavyo vya Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD kwa mwaka 2023: Kuwezesha upangaji wa pamoja kati ya idara na programu za AUC na AUDA-NEPAD kuhusiana na programu husika na kufanya kazi kama Sekretarieti ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD.

22. Zaidi ya hayo, Bibi Aïssatou Hayatou aliifahamisha Kamati Ndogo kwamba Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD kilifikia kiwango cha utekelezaji wa bajeti cha 98% kwa mwaka wa 2021, lakini kilibaini kupungua kwa kiasi kikubwa kwa mwaka 2022 kwa kiwango cha 10%. Kiwango cha chini cha utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa 2022 kilitokana na mkutano wa Kamati Ndogo kutofanyika na kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa kuajiri Vijana wa Kujitolea kwenye Kitengo cha Uratibu ambacho kilijumuisha 90% ya bajeti.

23. Pia, alipendekeza kwamba mgao wa fedha kwa ajili ya kuandaa Mkutano kwa ajili ya Kamati Ndogo urejeshwe kwenye bajeti ya Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD.

24. Kwa kuzingatia pendekezo lililotajwa hapo awali, Kamati Ndogo ilipendekeza kuongezwa kwa ukomo wa bajeti ya Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD ili kumudu gharama zinazohusiana na mkutano.

25. Katika mkutano wa 36 wa Kamati Ndogo ulioitishwa tarehe 23 Mei, 2023, taarifa muhimu zilitolewa kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) na Usalama wa Chakula barani Afrika. Mkutano huo, ulioongozwa na **Mhe. Victor Adekunle Adeleke**, Balozi wa Nigeria, ulijikita kwenye taarifa kuhusu mipango hii muhimu.

26. Taarifa kuhusu Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) na usalama wa chakula iliwasilishwa na **Mhe. Dkt.Ibrahim AssaneMayaki**, Mjumbe Maalumu wa Umoja wa Afrika anayehusika na Mifumo ya Chakula na aliyekuwa

Afisa Mtendaji Mkuu wa AUDA-NEPAD na Dkt. Manyewu Mutamba, Mkuu wa Kitengo cha Usalama wa Chakula, AUDA-NEPAD.

27. Katika wasilisho lake, **Mhe. Dkt. Ibrahim Assane Mayaki**, alisisitiza kuongezeka kwa umuhimu wa kisiasa na kijiografia wa chakula, alibainisha uwezekano wa matokeo chanya katika mfumo wa chakula wa Afrika kupitia utekelezaji wa sera na mabadiliko ya kimuundo, na kusisitiza hitaji muhimu la kuoanisha mipango kama vile CAADP, AfCFTA, na PIDA kwa ajili ya ukuaji mkubwa wa uzalishaji na usambazaji wa chakula katika ngazi ya kitaifa na bara.

28. Baada la wasilisho la **Mhe. Dkt. Ibrahim Assane Mayaki**, Dkt. Mutamba, alitoa taarifa kuhusu mipango ya sasa ya AUDA-NEPAD katika nyanja ya usalama wa chakula. Aliitaarifu Kamati Ndogo kwamba AUDA-NEPAD inashiriki kikamilifu katika kusaidia nchi wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs) kutekeleza michakato muhimu ya kiprogramu inayoshughulikia changamoto ya uzalishaji mdogo wa chakula katika bara.

29. Baada ya taaifa hizo, Kamati Ndogo ilitoa mapendekezo yafuatayo:

    I. Taasisi za maendeleo za Afrika zinapaswa kuchukua jukumu muhimu katika kuhamasisha uzalishaji wa chakula katika bara la Afrika.
    II. Usalama wa chakula unapaswa kuzingatiwa kama juhudi shirikishi zinazohusisha uoanishaji wa CAADP, PIDA, na AfCFTA, kwa kutambua uhusiano wa mipango hii.
    III. Inashauriwa kwa Nchi Wanachama kupitia na kurekebisha vipaumbele vyao vya Kitaifa vya Kilimo kwa kuzingatia utaalamu uliopo na mabadiliko ya hali ya Usalama wa Chakula barani Afrika.
    IV. Nchi za Kiafrika zinapaswa kuweka kipaumbele kwenye biashara ya mbolea miongoni mwao badala ya kuzisafirisha nje ya bara hili ili kukuza uwezo wa kujitegemea na tija kwenye kilimo.

30. Mkutano wa 37 wa Kamati Ndogo ulifanyika kwa njia ya mtandao tarehe 1 Juni 2023. Lengo kuu la mkutano lilikuwa kupokea taarifa kuhusu maendeleo ya Mpango wa AUDA-NEPAD wa 100,000 MSMEs (Biashara Ndogo ndogo, Ndogo na za Kati). Mkutano huo uliongozwa na Makamu Mwenyekiti wa kwanza wa Kamati Ndogo, Mhe. Mheshimiwa Abdi Mahamoud, Balozi wa Djibouti.

31. Mawasilisho kuhusu Mpango wa MSMEs 100,000 yalifanywa na Bi. RonOsman Omar, Kaimu Mkuu wa Maendeleo ya Uchumi, Utalii, Biashara, Viwanda, Madini (ETTIM), AUC, na Bi. Sara Ferdjani, Afisa Programu Mwandamizi wa AUDA-NEPAD.

32. Katika wasilisho lake, Bi. Sara Ferdjani alitoa taarifa ya Mpango wa Wafanyabiashara 100,000 wenye lengo la kukuza ajira barani Afrika kwa kuwezesha Biashara Ndogo ndogo, Ndogo na za Kati 100,000 (MSMEs). Mpango huo unajumuisha vipengele vinne muhimu:

I. Chuo cha MSME
II. Mpango wa Msaada wa Ufadhili wa MSME
III. Soko la MSME
IV. Jukwaa la Kidigitali la MSME

33. Baada ya mawasilisho kuhusu Mpango wa MSMEs 100,000, Kamati Ndogo ilitoa mapendekezo yafuatayo:

I. Mpango huo unapaswa kuhakikisha ushirikishwaji wa kiwango kikubwa wa wanawake na vijana katika sera zote za utekelezaji, kwa kutambua umuhimu wa ushiriki wao katika shughuli za mpango huo.
II. Mpango huo unapaswa kusaidia wajasiriamali wachanga, ili kuhakikisha kuwa wanapewa fursa za kifedha zinazoweza kufikiwa na huduma za mikopo kwa viwango na riba ndogo.
III. Mpango huu unapaswa kuzingatia mafunzo na juhudi za kujenga uwezo, kuwezesha biashara hizi kukuza ujuzi na uwezo wao.
IV. Uratibu kati ya AUDA-NEPAD na Idara ya ETTIM unapaswa kuimarishwa ili kufikia matokeo bora zaidi.

34. Tarehe 5 Juni 2023, Kamati Ndogo ilifanya kikao cha kujitambulisha huko Addis Ababa, Ethiopia, kilichoongozwa na **Mhe. Balozi Abdi Mahamoud**. Kikao hicho kililenga kuwafahamisha wajumbe wapya kuhusu mawanda ya kazi ya Kamati Ndogo, kuhakikisha wanajitayarisha kutekeleza majukumu yanayohusiana na ujumbe wao kwa ufanisi.

35. Wakati wa kikao cha utambulisho **Bw. Mohamed Abdisalam**, Mkurugenzi wa Uendeshaji wa AUDA-NEPAD, alitoa taarifa ya kina ya historia ya taasisi, mfumo wa kitaasisi na taratibu za kanuni na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uratibu, Bi. Aïssatou Hayatou alitoa taarifa kuhusu ajenda na mpangokazi wa Kamati Ndogo.

36. Mkutano wa 39 wa Kamati Ndogo wa tarehe 28 Julai 2023, uliongozwa na **Mhe. Abdi Mahamoud**, alipitia programu yake ya kazi kwa mwaka. Hivyo, Kamati Ndogo ilipendekeza kuongeza kipengee cha ajenda kuhusu maandalizi ya kaulimbiu ya mwaka 2024 kuhusu Elimu.

37. Mkutano wa 40 wa Kamati Ndogo ulifanyika kwa njia ya mtandao tarehe 10 Oktoba 2023. Lengo kuu la mkutano huu lilikuwa kupokea taarifa fupi kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Miundombinu Barani Afrika: Mpangokazi wa Kipaumbele (PIDA). -PAP 2). Mkutano huo uliongozwa na **Mhe. Daniel Owassa**, Balozi wa Kongo, kwa nafasi yake kama Kaimu Mwenyekiti wa Kamati Ndogo.

38. Taarifa kuhusu PIDA PAP 2 ziliwasilishwa na **Dkt. Amine Idriss Adoum** Mkurugenzi wa Utekelezaji wa Programu & Uratibu, AUDA-NEPAD na **Bw. Kamugisha Kazaura**, Mkurugenzi wa Miundombinu na Nishati, AUC akisaidiwa

na Bw. Ayoub Chajadine, Mratibu wa Mpango wa Maendeleo ya Miundombinu Afrika (PIDA), AUC.

39. Taarifa hiyo ilisisitiza umuhimu wa kuongeza fedha na rasilimali za kitaalamu za Nchi Wanachama, kuimarisha ushirikiano na wadau, kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi, na kujenga uwezo wa kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa PIDA, ikiwa ni pamoja na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

40. **Dkt. Amine** pia alipendekeza kuwa Nchi Wanachama zifikirie kuwekeza katika PIDA na kutoa msaada kwa mfumo ulioanzishwa wa PIDA wa kutoa huduma, ambao una jukumu la kufanya upembuzi yakinifu katika miradi ya PIDA. Kwa sasa unasimamia upembuzi yakinifu kwa miradi 22 kati ya 69 ya PIDA. Kwa bahati mbaya, utegemezi wa sasa wa ufadhili kutoka kwa wabia wa maendeleo pekee unaleta changamoto kwa uendelevu wa mfumo huu.

41. Mkutano wa 41 wa Kamati Ndogo ulifanyika tarehe 14 Novemba 2023. Ajenda ya msingi ilihusisha kubadilishana mawazo kuhusu hali ya maandalizi ya kaulimbiu ya Mwaka 2024: “Elimisha Mwafrika anayefaa kwa Karne ya 21: Kuweka mifumo ya elimu stahimilivu ili kuongeza upatikanaji wa elimu jumuishi, ya kudumu , bora, na inayofaa barani Afrika”, pamoja na kutoa taarifa kuhusu Mfuko wa Maendeleo na Utafiti wa Upembuzi Yakinifu kuhusu Fedha Zisizotumika kutoka kwa Wabia wa Kimataifa. Mkutano huo uliongozwa na **Mhe. Mheshimiwa Abdi Mahamoud**, Balozi wa Djibouti.

42. . Taarifa kuhusu kaulimbiu ya mwaka 2024 kuhusu Elimu, iliwasilishwa na Bi. Unami Dube, Afisa Programu Mwandamizi wa masuala ya ufundi stadi (WorldSkills Africa and Skills Initiative for Africa Financing Facility) katika AUDA-NEPAD, na Bi. Sophia Ndemutila Ashipala, Mkuu wa Kitengo cha Elimu katika AUC. Mkurugenzi wa Uendeshaji wa AUDA-NEPAD **Bw. Mohamed Abdisalam** alitoa taarifa kuhusu Mfuko wa Maendeleo wakati wa mkutano huo.

43. Katika wasilisho lake, Bi. Sophia alitoa alijikita katika mada kuu za mwaka 2024. Alipendekeza kwamba Kamati Ndogo izihamasishe Nchi Wanachama ili kutekeleza kikamilifu matamko yaliyoainishwa katika malengo ya CESA na SDG, ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu. Aidha, Bi. Sophia alisisitiza haja ya kutatua changamoto zinazohusiana na ufadhili wa elimu.

44. Bi Unami pia alitoa ujumbe muhimu ufuatazo wa uhamasishaji kwa ajili ya kujadiliwa na Kamati Ndogo:
    I. Kujenga mifumo ya stadi na ajira inayoweza kubadilika kwa urahisi ili kushughulikia viwango vya juu vya ukosefu wa ajira kwa vijana
    II. Kuboresha sera na mifumo ya udhibiti ili kuweka mazingira wezeshi ya mabadiliko ya mifumo ya Elimu ya Ufundi Stadi (mtaala unaozingatia mahitaji; uanagenzi; n.k)
    III. Kuboresha utawala na uratibu wa mifumo ya mafunzo ya ufundi na taaluma
IV. Kuhamasisha sekta zinazoendeshwa na kuzingatia mahitaji ya kikazi ya sekta

V. kuongeza uwezo wa kuajiriwa kwa vijana
VI. Kuimarisha mikakati na mifumo ya makadirio ili kujenga uhusiano bora wa mifumo ya mafunzo ya ufundi kwa mahitaji ya soko la ajira.
VII. Nchi Wanachama wa taasisi ya Rally kujiunga na taasisi ya WorldSkills Africa (Zambia, 2025)

45. Kuhusu upembuzi yakinifu wa Mfuko wa Maendeleo, **Bw. Abdisalam** aliitaarifu Kamati Ndogo kuhusu kukamilika kwake. Ripoti itashirikishwa kwa Nchi Wanachama baada ya tathmini na mapitio ya menejimenti ya AUDA-NEPAD. **Bw. Abdisalam** alibainisha upungufu mkubwa katika tathmini ya FTYIP: ukosefu wa uchanganuzi wa kina wa gharama, na kusababisha changamoto katika kubainisha kwa usahihi rasilimali fedha zinazohitajika kwa utekelezaji wenye ufanisi. Tatizo hili lilizuia upangaji na ugawaji wa rasilimali, na hivyo kufanya kuwa vigumu kutathmini upungufu wa fedha. Hivyo, STYIP imeboresha makadirio ya gharama kwa Afrika yakioana na malengo ya kuharakishwa na ufadhili endelevu katika muongo ujao. Upembuzi yakinifu uliokamilishwa utashirikishwa kwa Nchi Wanachama ifikapo mwisho wa mwaka.

46. Zaidi ya hayo, **Bw. Mohamed Abdisalam** alitoa wito kwa Nchi Wanachama kujitolea zaidi kwa wakati mwafaka, kwa ajili ya ufanisi wa jumla wa Mfuko. Ili kuongeza upatikanaji wa fedha na kuvutia vyanzo vya ziada vya mtaji, alipendekeza kuboresha mwonekano wa kipekee wa mfuko ili kuendesha na kuharakisha vipaumbele vya STYIP. Hii inatoa fursa muhimu kwa AUDA-NEPAD na mfuko kujiweka kimkakati kama viongozi katika kuendeleza ajenda muhimu ya mabadiliko ya bara kwa miaka kumi ijayo na zaidi.

47. Mkutano wa 42 na wa mwisho wa Kamati Ndogo ulifanyika tarehe 1 Desemba 2023, kwa njia ya mtandao na uliongozwa na **Mhe. Abdi Mahamoud**, Balozi wa Djibouti. Ajenda kuu ya mkutano huu ilikuwa kuangalia maendeleo katika utekelezaji wa kaulimbiu ya Mwaka 2023: “Kuharakisha utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika”. Kamati Ndogo pia ilijadili Rasimu ya Ripoti yake ya Mwaka ya 2023, ambayo itawasilishwa kwenye Mkutano wa Kawaida wa PRC uliopangwa kufanyika Januari 2024.

48. Mawasilisho kuhusu kaulimbiu ya mwaka 2023 ya AfCFTA, yalifanywa na Bw. Million Habte, Mratibu wa utekelezaji wa AfCFTA na Kaimu Mkuu wa Ofisi ya Uhusiano ya AfCFTA, Bw. Mustafa Sakr, Mkuu wa Biashara na Masoko katika AUDA- NEPAD, na Bw. Chiza Charles Newton, Kaimu Mkurugenzi wa Viwanda, Ujasiriamali wa Madini, na Utalii katika Idara ya Maendeleo ya Uchumi, Utalii, Biashara, Viwanda, Madini (ETTIM), AUC.

49. Katika wasilisho lake, Bw. Million alijikita kwenye juhudi zilizochukuliwa na Sekretarieti ya AfCFTA ili kuwezesha majadiliano na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa AfCFTA, kwa kushirikiana na Umoja wa Afrika (AU), ikiwa ni sehemu ya kutangaza Kaulimbiu ya Mwaka ya AU. 2023: "Kuharakisha

Utekelezaji wa AfCFTA." Kupitia shughuli hizi Sekretarieti ya AfCFTA ilirekodi mafanikio yafuatayo:

I. Nchi 47 kati ya 54 Wanachama wa UA ziliridhia Mkataba wa AfCFTA.
II. Mfumo wa Usuluhishi wa Migogoro wa AfCFTA ulianza kufanya kazi, na mazungumzo ya Awamu ya 2 yalihitimishwa kwa kupitishwa kwa hati tatu za kisheria.
III. Nchi 5 Wanachama ziliteuliwa kuingia kwenye Baraza la Rufaa, chombo muhimu cha Usuluhishi wa Migogoro ya Bara, na juhudi zinaendelea za kujaza nafasi mbili zilizosalia.
IV. Utekelezaji wa Kitaifa wa Mkataba wa AfCFTA umeanza katika Nchi 25 Wanachama na Jumuiya moja ya Kiuchumi ya Kanda na takriban Kamati 20 za Kitaifa za Utekelezaji wa AfCFTA ziliundwa ili kuimarisha ushirikiano mzuri na wadau mbalimbali ili kusaidia utekelezaji wa AfCFTA kwa kuzingatia Kaulimbiu ya Mwaka 2023.
V. Mfuko wa Maboresho wa AfCFTA, wenye makao yake makuu mjini Kigali, Rwanda ulipokea ahadi ya dola bilioni 1 kutoka kwa Afreximbank, kama mchango kwenye lengo la dola bilioni 10 kwa ajili ya ufadhili wa utekelezaji wa AfCFTA. .

50. Bw. Mustafa Sakr alisisitiza kwamba, kwa kuzingatia Kaulimbiu ya Mwaka, AUDA-NEPAD inatambua jukumu muhimu la AfCFTA na imebainisha vipaumbele muhimu vinavyolenga kuimarisha uhusiano uliojengwa kati ya AfCFTA na taasisi nyingine, kama PIDA.

51. Kuhusiana na AfCFTA, AUDA-NEPAD iliainisha maeneo ya utekelezaji, ikiwa ni pamoja na tathmini ya mahitaji ya wadau, kuwezesha biashara, kukuza uwezo, uchanganuzi wa biashara ya Afrika na kuongeza upatikanaji wa soko. Mafanikio makubwa katika mwaka 2023 ni pamoja na: kuandaa kwa mafanikio warsha kuhusu Kuharakishwa kwa Maendeleo ya Viwanda barani Afrika (AIDA)/AfCFTA Tathmini ya Athari, kuandaa uthibitisho wa dhana ya manufaa ya ICT katika vituo vya mpakani vya Zambia, na kuchangia katika kukuza uwezo wa mipango kama vile Nishati kwa Africa. Maendeleo pia yanaonekana katika utekelezaji wa Mpango wa Stadi kwa Afrika (SIFA), hususan Mfuko wa Ufadhili wa SIFA katika nchi nane za Afrika.

52. Bw. Chiza Charles Newton kwa upande wake alibainisha kuwa Idara ya ETTIM imechangia kwa kiasi kikubwa katika Kaulimbiu ya Mwaka kupitia mipango kama vile kuandaa Mwongozo wa utekelezaji wa matokeo kutoka kwa Mkutano Usio kwenye ratiba wa UA kuhusu ukuaji wa viwanda. Juhudi nyingine ni pamoja na kuzindua tafiti kuhusu maendeleo ya mauzo ya nje, uandaji wa Miongozo ya UA ya Kutunga Sera Shirikishi ya Biashara, na Mkakati wa Umoja wa Afrika wa Madini ya Kijani. ETTIM pia imeshiriki katika mipango kama vile Programu ya Wanawake Wanaochakata Afrika (AWIP), Miundombinu Bora Barani Afrika, na Maonyesho ya Tatu ya Biashara ya Ndani ya Afrika.

53. Baada ya mawasilisho yao, watoa mada waliwasilisha mapendekezo yafuatayo ili yajadiliwe na Kamati Ndogo:
    I. Nchi Wanachama zinapaswa kuweka kipaumbele na kutenga rasilimali fedha zaidi kwa shughuli za AfCFTA na kupunguza utegemezi kwa Wabia wa Maendeleo.
    II. Kuzingatia kutambulishwa kwa kaulimbiu ndogo za UA pamoja na kaulimbiu ya mwaka kwa muda mrefu zaidi ya kipindi cha sasa cha mwaka mmoja kwa utekelezaji mzuri na manufaa zaidi.
    III. Kuimarisha juhudi za utetezi na uhamasishaji wa AfCFTA na programu zinazohusiana nazo katika ngazi ya kitaifa.

D. Mahitimisho

54. Katika mwaka 2023, kupitia mazungumzo kati ya AUDA-NEPAD, Kamisheni ya UA na watendaji wengine ndani ya mfumo wa UA, Kamati Ndogo ilipata fursa ya kuthamini maendeleo yaliyofikiwa na taasisi na Nchi Wanachama wa UA katika utekelezaji wa Ajenda 2063, kwa msisitizo maalumu kwenye programu na mipango muhimu ya kipaumbele.

55. Wakati UA inaelekea kupitisha Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi wa Ajenda ya 2063, katika mazingira yenye changamoto Barani ambayo yanahusiana na sababu za ndani na, kwa kiasi kikubwa, na maendeleo katika nyanja ya kimataifa, taasisi za UA na Nchi Wanachama zinalazimika kuongeza juhudi zao kwa kiasi kikubwa, ili kufanikiwa kutekeleza dira ya Bara lenye amani na ustawi.

56. Kamati Ndogo inathamini maendeleo yaliyopatikana katika uratibu kati ya AUC na AUDA-NEPAD kama ilivyobainishwa katika taarifa za pamoja zilizotajwa katika hili ripoti, ambayo yamesababisha ushirikiano mzuri, upangaji bora, na utumiaji sahihi wa rasilimali.

57. Hata hivyo, wasiwasi unabakia kuhusu uwezo wa kitaasisi na kifedha wa AUDA-NEPAD na AUC, ili kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Zaidi ya hayo, kuingizwa kwa AU kwenye G20, na upanuzi wa BRICS na kujuimuisha nchi zaidi za Kiafrika inaashiria kwamba uandaaji wa mikakati na sera ambazo zitaongoza na kuunga mkono mazungumzo ya Afrika katika nyanja ya kimataifa kwa muda wa kati na mrefu, umekuwa jambo la lazima, ikiwa Afrika itafanikiwa kulinda rasilimali zake, kuziendeleza na kuzibadilisha kuwa vyanzo vya ustawi kwa kizazi kijacho cha Waafrika.

58. Mafunzo yaliyopatikana kutokana na athari mbaya za janga la UVIKO-19, pamoja na mambo mengine, yanabainisha hitaji muhimu la Afrika kuimarisha taasisi zake katika Serikali, na vile vile ngazi ya bara, ili kuongeza utegemezi wake katika vyanzo vya ndani vya fedha kwa ajili yake Ajenda ya ushirikiano na maendeleo. Hivyo, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo na kupitishwa kwa

Bajeti ya miaka tofauti kwa UA ni fursa za kuimarisha kwa kiasi kikubwa matokeo ya programu na sera.

59. Hivyo, mwaka wa 2024, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati Ndogo itajaribu kuweka mwelekeo mpya kuhusiana na jukumu lake la utetezi. Kwa maana hiyo, Kamati Ndogo inakusudia kuanzisha uhusiano wa mara kwa mara na wadau, kwa nia ya kuipa taarifa Kamati Ndogo kuhusu masuala muhimu, kuimarisha ushirikiano na kuoanisha maoni na vyombo vingine vya sera, hususani, Kamati Maalumu ya NEPAD, na Kamati ya Mabalozi kuhusu Ajenda ya 2063, pamoja na kuorodhesha michango ya RECs na kuhamasisha wabia wa Kimataifa.

E. Mapendekezo

60. Kamati Ndogo inaiomba PRC kuzingatia mapendekezo yafuatayo:

a) Kuiomba AUDA-NEPAD kuwasilisha upembuzi yakinifu wa Mfuko wa Maendeleo kwa vyombo vinavyohusika vya UA kwa ajili ya mapitio na kupitishwa, kwa mujibu wa Uamuzi wa Baraza la Utendaji 1143 (Februari 2022) na hivyo, kutoa mwelekeo unaohusiana na sekta za maendeleo ya kimkakati ndani ya Mfumo wa Mfuko wa Maendeleo, ili kuepusha uongezaji wa fedha, kulingana na kikomo kilichopitishwa na Baraza la Utendaji;

b) Kuanzisha, kupitia Uamuzi wa Baraza la Utendaji, mkutano wa kila mwaka wa Kamati Ndogo na AUDA-NEPAD;

c) Pia Kuanzisha mkutano wa pamoja kati ya Kamati Ndogo ya NEPAD, Kamati ya Mabalozi kuhusu Ajenda 2063 na Kamati Maalumu ya NEPAD;

d) Kusaidia uimarishaji wa uwezo wa kitaasisi wa Sekretarieti ya Kamati Ndogo (Kitengo cha Uratibu) kupitia utekelezaji wa haraka wa muundo wake;

e) Kwa kuzingatia viwango vyao vilivyobaki vya utekelezaji wa bajeti (AUDA-NEPAD 98% kwa mwaka 2022, Kitengo cha Uratibu 100% 2023):

- kuidhinisha mapitio ya ukomo wa bajeti ya AUDA-NEPAD na Kitengo cha Uratibu ili kuongeza mgao wao wa bajeti ili kushughulikia shughuli zinazopendekezwa;
- Kuunga mkono ongezeko la Bajeti ya AUDA-NEPAD kama kipaumbele huku ikitoa elimu kwa wabia kuhusu umuhimu wa kuongeza msaada wao wa kifedha na kitaalamu kwa manufaa ya Taasisi;

f) Kuhusu Masuala matatu muhimu: Amani, Usalama na Maendeleo, wito kwa Taasisi kufanya kazi kwa karibu na Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama katika suala hili muhimu ili kukuza ushirikiano, hususani, ili kuepuka kuandaa mikutano kadhaa ya Kiafrika kuhusiana suala hilo hilo;

g) Kurejelea haja ya kuimarisha uratibu kati ya vyombo vya Umoja wa Afrika na kuhimiza, katika suala hili, AUDA-NEPAD kuendelea na mashauriano

na vyombo vinavyohusika vya Umoja wa Afrika kwa nia ya kuoanisha Mipango ya utekelezaji ya kila mwaka na kuepuka kurudiwa;

h) Kujumuisha taarifa za nusu mwaka kuhusu AUDA-NEPAD kwenye Ajenda ya PRC. /..

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-02-15

Report of the Sub-Committee on NEPAD

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10501

Downloaded from African Union Common Repository